

# THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA



**For Competitive, Efficient, Quality and Safe Transport Services**

Surface and Marine Transport Regulatory Authority  
Mamlaka ya Udhhibiti Usafiri wa Nchi Kavu na Majini

## **TAARIFA KWA WAMILIKI WA MABASI UTOAJI WA LESENI KWA MAKAMPUNI YA USAFIRISHAJI WA UMMA JIJINI DAR-ES-SALAAM.**

Mamlaka ya Udhhibiti Usafiri wa Nchi Kavu na Majini (SUMATRA) inapenda kuwatangazia wadau wa sekta ya usafirishaji kuwa utaratibu wa kutoa leseni kwa makampuni ya usafirishaji unatarajiwa kuanza tarehe 1 Januari 2016.

SUMATRA ilianzisha mpango huu ikiwa na njia mojawapo ya kuboresha utoaji huduma za usafiri kutokana na kutoridhishwa na utoaji huduma wa Dar-es-Salaam ambapo kumekuwa hakuna utaratibu wa wamiliki kuwasimamia madereva na makondakta wao na hivyo kuchangia uvunjifu wa sheria na kanuni za usalama barabarani pamoja na utoaji wa huduma ya usafiri hafifu.

Uhamasishaji wa uundwaji wa makampuni hayo ulianza tangu mwaka 2010 kwa kuandaa mkutano ulioandaliwa na SUMATRA kwa ajili ya kupata maoni ya wadau wa sekta ya usafirishaji.

Mfumo huu wa makampuni ya usafirishaji una manufaa makubwa kwa mmiliki kama vile kuwa na wakaguzi wao binafsi ambao pamoja na kudhibiti matumizi mabaya ya magari yao na kudhibiti uvujaji wa mapato ya kampuni.

Huduma ya usafiri kupitia makampuni ina manufaa kama yafuatayo;

- Uwezekano wa kupata menejimenti ya kisasa na yenye taaluma katika mambo ya usafirishaji.
- Makampuni kuweza kuandaa taarifa za kihasibu na kuwa na utaratibu wa kuweka pesa benki na kumudu kununua vyombo bora vya usafiri.
- Ni rahisi kupata mikopo ya kununua magari ikiwemo pia mikopo ya muda mfupi kugharamia gharama za uendeshaji.
- Utaratibu nafuu wa bima ya magari na mengineyo mengi.

Pia itasaidia wamiliki kufanya biashara ya usafirishaji kwa weledi na ufanisi zaidi na kumuwezesha mhibiti kuwasimamia watoa huduma wachache na hivyo kuwa na usafiri bora kwa wananchi wa Tanzania.

SUMATRA inawataka wamiliki wa vyombo vya usafiri hususani wa mabasi yanayotoa huduma za usafiri mijini kuondoa hofu na kubadilika kwa kuungana pamoja kuanzisha makampuni au ushirika kwa ajili ya maslahi ya muda mrefu na yenye tija kwao na kwa sekta ya usafirishaji wa abiria nchini.

Kwa ufafanuzi na maelekezo zaidi unashauriwa kufika katika Ofisi ya Mkurugenzi wa Udhibiti Usafiri wa Barabara, SUMATRA Makao Makuu iliyoko katika makutano ya Barabara ya Ali Hassani Mwinyi na Mtaa wa Nkomo, Upanga Dar es Salaam. Aidha unaweza kuwasiliana na Mamlaka kwa kupitia **Simu Na. 2197500/501, Nukushi: 2116697**, Barua pepe: [dg@sumatra.go.tz](mailto:dg@sumatra.go.tz) au [infor@sumatra.go.tz](mailto:infor@sumatra.go.tz) .

Imetolewa na:

Ofisi ya Mkurugenzi Mkuu,

SUMATRA,

S.L.P 3093,

DAR ES SALAAM

Tovuti: [www.sumatra.go.tz](http://www.sumatra.go.tz)